**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**

**TUME YA MIPANGO**

# MAFANIKIO YA MIAKA MITATU YA UONGOZI WA RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

**MACHI 2024**

## I. UTANGULIZI

1. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliingia madarakani Machi 19, 2021. Baada ya kuapishwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, alilihutubia Bunge la 12 Aprili 22, 2021, ambapo aliwaahidi watanzania kuwa Serikali ya Awamu ya Sita **itadumisha mazuri yaliyoanzishwa katika Awamu zilizopita, kuendeleza mema yaliyopo na kuleta mengine mapya**. Aidha, Mheshimiwa Rais alibainisha kuwa azma ya kudumisha, kuendeleza na kuleta mambo mazuri mapya ni kutekeleza kwa vitendo dhana na maana halisi ya kaulimbiu ya **"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Kazi Iendelee"**. Kwa msingi huo, Mheshimiwa Rais aliahidi umma wa watanzania kuwa ataenzi na kuendeleza mambo yote mazuri; na kufanya mabadiliko pale itakapobidi kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

2. Kutokana na azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliunda Tume ya Mipango mnamo **tarehe 15 Julai, 2024** kwa lengo la kutatua changamoto za Wizara za kisekta kutopanga kwa pamoja, kukosekana kwa mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini ya mipango na miradi ya maendeleo; kukosekana kwa mfumo rasmi wa kupata taarifa za uwekezaji wa sekta binafsi; kutofungamanishwa kwa mipango mikakati ya kisekta na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Hivyo, Tume ya Mipango imeanzishwa ikiwa na jukumu la msingi la kusimamia uchumi, mchakato wa upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa kama ilivyoidhinishwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa kunakuwa na ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa na maendeleo kama ilivyokusudiwa.

## II. MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA USIMAMIZI WA UCHUMI NA MCHAKATO WA UPANGAJI

3. Serikali ya Awamu ya Sita inatimiza miaka mitatu Machi 18, 2024 tangu iingie madarakani. Aidha, kwa kuzingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais ya **kuhakikisha Taifa inakuwa na maendeleo endelevu kupitia kubainisha hali halisi ya maendeleo ya nchi, changamoto na fursa; kubainisha mwelekeo wa nchi kimkakati kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na muda mrefu, malengo na mikakati ya utekelezaji; na kuongoza maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050**, Tume ya Mipango imeweza kupata mafanikio yafuatayo: -

**Ubainishaji wa Hali Halisi ya Maendeleo ya Nchi**

4. Katika kuhakikisha nchi inakuwa na Maendeleo endelevu, Serikali ya awamu ya sita imeweza kufanya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ili kuweza kuainisha bayana maendeleo yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Kwa ujumla utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 umefanikiwa kwa asilimia 60 hadi kufikia mwaka 2022 ambapo mafanikio makubwa yamepatikana katika sekta za huduma ya jamii. Mafanikio hayo yametokana na:

a) **Kuboreka kwa maisha Bora kwa kila mtanzania;**

i. **Usalama wa Chakula na lishe**

Tanzania kwa ujumla imefanikiwa kuongeza uwiano wa chakula kutoka chini ya asilimia 110 mwaka 1990 hadi kufikia kati ya asilimia 114 na 120 mwaka 2020 ambapo usalama wa chakula umeweza kufikia asilimia 10.7. Hali hii imethibitika kutokana na kupungua kwa idadi ya watoto walio chini ya miaka mitano wana wanaoteseka na utapiamlo na uzito pungufu kutoka asilimia 48.3 na 25.3 mwaka 1999 hadi asilimia 30 na 12 mwaka 2022, mtawalia.

ii. **Elimu ya Msingi**

Nchi imefanya maendeleo makubwa katika kufikia lengo la kufikia usajili wa shule za msingi kwa wote kutokana na uwekezaji uliofanywa na Serikali, sekta binafsi, na mashirika ya kidini, pamoja na jitihada za kuendelea kuhakikisha uwiano unaofaa kati ya walimu na wanafunzi, pamoja na idadi ya vitabu vya msingi na madawati ya kukaa darasani. Kiwango cha usajili kwa shule ya msingi kimeongezeka kutoka asilimia 69 mwaka 1999 hadi kufikia asilimia 97 mwaka 2022. Kufuatia mafanikio haya, Serikali iliongeza kiwango cha chini cha elimu ya msingi ya lazima kutoka kiwango cha saba cha msingi hadi kiwango cha elimu ya sekondari cha kidato cha nne ifikapo mwaka 2025. Kwa ujumla, upatikanaji wa elimu ya msingi kwa wote imekua kwa asilimia 23.6.

iii. **Upatikanaji wa huduma Bora ya afya ya msingi**

Kwa ujumla kiwango cha upatikanaji wa huduma bora ya afya ya msingi imekua kwa asilimia 21.6 mwaka 2022. Hali hii imetokana na uwepo wa vituo vya afya vinavyotoa huduma na dawa muhimu zinazoweza kudumu kwa mrefu kuongezeka kutoka asilimia 64 mwaka 2015 hadi asilimia 78 mwaka 2022, uwepo wa hospitali za rufaa za kitaifa na kikanda zinazotoa huduma za matibabu ikiwemo utalii wa matibabu katika baadhi ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Maendeleo yamefanywa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa kukuza bima ya afya ya kimataifa kwa kila raia na kuhakikisha zahanati inapatikana katika kila kijiji.

### iv. Upatikanaji wa huduma bora ya afya ya Uzazi

Lengo lilikuwa kupunguza vifo vya wamama wajawazito kutoka vifo 600 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2000 kufikia vifo 265 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2025. Hadi kufikia mwaka 2020, idadi ya vifo vya wamama wajawazito ilipungua na kufikia takriban vifo 235 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2020 kutoka vifo zaidi ya 750 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2000. Hii imetokana na kuongezeka kwa kiwango cha wanawake wanaopata huduma za uzazi wa kabla ya kujifungua kutoka chini ya asilimia 40 mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 65 mwaka 2022.

### v. Kupungua kwa vifo vya watoto wachanga

Lengo lilikuwa kupunguza kiwango cha vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 85 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2000 na kufikia vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000 na kupunguza kiwango cha vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano kutoka vifo 112 kwa kila vizazi hai 1,000 kufikia vifo 57 kwa kila vizazi hai 1,000 katika nchi za kipato cha kati cha chini. Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka takriban vifo 85 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2000 hadi takriban vifo 36 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2022. Vilevile, kiwango cha vifo cha watoto chini ya umri wa miaka mitano kimepunguzwa hadi vifo 49 kwa kila vizazi hai 1,000, ikilinganishwa na takriban vifo 130 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2000. Asilimia ya watoto wanaozaliwa wafu pia imepungua kutoka takriban vifo 25.9 kwa kila vizazi 1,000 hadi vifo 18.6 kwa kila vizazi 1,000. Mafanikio yaliyorekodiwa yanatokana na programu za kitaifa za chanjo kubwa dhidi ya magonjwa ya kuambukiza wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua na mafunzo ya idadi ya kutosha ya wakunga rasmi na wasio rasmi ili kuhudumia vijiji vingi iwezekanavyo.

### vi. Upatikanaji wa maji safi na salama

Lengo lilikuwa kuongeza asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji yaliyotiririka au maji yaliyolindwa kama chanzo chao kikuu kutoka asilimia 50 mwaka 2000 hadi asilimia 85 ifikapo mwaka 2025. Lengo linalolingana kwa idadi ya watu wa mijini ni asilimia 95. Hadi kufikia Desemba 2022, asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji safi na salama ilikuwa imefikia asilimia 77, wakati katika maeneo ya mijini, ilikuwa imefikia asilimia 88. Mafanikio haya yametokana na uwepo wa mfuko maalum wa maji na vyanzo thabiti na vinavyoweza kutabirika unaosimamiwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na Mjini (RUWASA).

### vii. Kiwango cha maisha (Umri wa Kuishi)

Lengo lilikuwa ni kuongeza kiwango umri wa kuishi kutoka miaka 52 mwaka 2000 hadi kufikia miaka 68 mwaka 2025. Hadi kufikia mwaka 2022, kiwango cha umri wa

kuishi kwa watanzania kilikuwa kimefikia miaka 66 kutokana na nchi kuwekeza katika masuala muhimu ikiwemo upatikanaji wa elimu, huduma za afya ya msingi, huduma za afya kwa kina mama na upatikanaji wa maji safi.

**b) Utawala Bora**

Katika lengo hili mafanikio yaliyopatikana ni kuboreka kwa upatikanaji wa haki kutokana na maboresho yaliyofanywa na mahakama katika kushughulikia mashauri kwa asilimia 22.6, utekelezaji wa sheria na kanuni asilimia 12.3, ulinzi wa haki za binadamu asilimia 12.4 na uwazi na uwajibikaji katika taasisi za umma asilimia 10.2. Mafanikio haya yamejidhihirisha katika ukomavu wa mfumo wa kidemokrasia wa nchi wakati wa Serikali ya Awamu ya Sita ilipoingia madarakani.

**c) Kujenga Uchumi Imara na Shindani katika Msingi wa Viwanda**

Kiwango cha wastani wa ukuaji wa Pato la Taifa kati ya mwaka 2000 na 2021 kilikuwa asilimia 6.7 kwa mwaka. Mchango wa sekta za viwanda, ujenzi na uzalishajikatika pato la taifa umeongezeka kutoka asilimia 24.3 mwaka 2000 hadi asilimia 35.6 mwaka 2022. Katika kipindi chote cha tathmini, mfumuko wa bei ulibaki kuwa tarakimu moja.

Vilevile, mauzo nje ya nchi kutokana na bidhaa za viwandani yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 43.1 mwaka 2000 hadi Dola za Marekani milioni 1,321 mwaka 2022. Hali hii imechangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji wa kimkakati, hususan katika miundombinu ya nishati ya umeme, maji, afya, elimu, ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege, teknolojia ya mawasiliano. Maeneo mengine ni kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

5. Mafanikio haya yametokana na *agizo la Mheshimiwa Rais lililotolewa mwaka 2022 kwamba angalau asilimia 80 ya Watanzania wawe na upatikanaji wa nishati safi na salama ya kupikia ifikapo mwaka 2032.* Vilevile, uwekezaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) umewezesha kuanzishwa kwa elimu kwa njia ya mtandao (e-learning), tiba kwa njia ya mtandao (e-medicine), huduma za sheria kwa njia ya mtandao (e-justice), na utoaji wa huduma za serikali kwa njia ya mtandao (e-government), pamoja na majukwaa ya mtandaoni kwa huduma kama usimamizi wa fedha za umma, utawala wa mapato, usimamizi wa rasilimali watu, mifumo ya malipo, usajili wa biashara, bima, elimu na afya. Mageuzi makubwa yamefanyika katika uingizaji wa kifedha ulioletwa na huduma za pesa za mkononi ambapo hadi mwaka 2021/22, kulikuwa na jumla ya akaunti 34,971,596 za mifuko ya pesa za mkononi zilizokuwa zinaendeshwa kwa shughuli, na thamani ya soko la simu ya mkononi ilikuwa TZS 1,158.5 bilioni.

6. Kuendelea kuimarika kwa viashiria vya uchumi jumla ni matokeo ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kufungua fursa fiche kupitia uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji, biashara na utalii (kupitia royal tour).

**Kubainisha Mwelekeo wa Nchi Kimkakati kwa Kipindi cha Muda Mfupi, wa Kati na Muda Mrefu, Malengo na Mikakati ya Utekelezaji;**

7. Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu ambayo inaainisha mwelekeo wa nchi kimkakati kupitia malengo na mikakati ya utekelezaji wake. Hii imejidhihirisha kupitia falsafa ya *"Usipojipangia Utapangiwa"* kwa kuandaliwa na kutekelezwa kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa mwaka 2021/22 – 2025/26. Mpango huu wa muda wa kati umeweka msukumo katika kuongeza uwezo wa uzalishaji kwa kujenga uchumi shindani utakaochochea ushiriki wa nchi katika biashara na uwekezaji na kuchochea maendeleo ya watu. Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umegawanyika katika mipango ya muda mfupi ya mwaka mmoja mmoja.

8. Uanzishwaji wa Tume ya Mipango umewezesha kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ya kipaumbele na kimkakati kupitia mipango ya muda wa kati na muda mfupi kwa kuhakikisha sekta zinashirikiana ipasavyo kupitia falsafa yake ya *Fikra za Pamoja na Utekelezaji Ulioratibiwa kwa Ustawi Jumuishi* ili kuweza kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa katika Dira ya Taifa wa Maendeleo ya 2025 ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati wa chini kwa kuwa na kiwango cha pato la Dola za Marekani 3,000 kwa kila mtu na kufanyika kwa shughuli za ufuatiliaji na tathmini za miradi ya maendeleo na mipango ili kuwepo kwa tija na matumizi bora ya rasilimali fedha, uzingatiaji wa mabadiliko ya tabianchi na mapinduzi ya nne ya viwanda (4th Industrial Revolution) yanayochagizwa na maendeleo ya kasi ya teknologia na mageuzi ya kidijitali kama vile matumizi ya akili bandia (Artificial Intelligence).

**Kuongoza maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050**

9. Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuanza kwa zoezi la maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 pamoja na Mpango Elekezi wa Muda Mrefu. Katika kuhakikisha kuwa zoezi hili linakuwa jumuishi na shirikishi, nyenzo na mbinu mbalimbali zimeandaliwa ambazo zitawezesha wananchi na wadau wengi kutoa maoni yao. Njia hizo ni pamoja na:

i. Utoaji wa maoni kwa kutumia simu ya aina yoyote (sio lazima simu janja) kupitia namba ya e-GA ya huduma za Serikali ya *152*00#. Hadi kufikia tarehe 3 Machi, 2024 maoni takribani 594,414 yalikuwa yamepokelewa

kupitia njia husika;

ii. Utoaji wa maoni kupitia tovuti maalum ya maoni ya Dira 2050 (https://dira2050portal.planning.go.tz/tume/dira). Hadi kufikia tarehe 3 Machi, 2024 maoni takribani 6,935 yalikuwa yamepokelewa;
iii. Mahojiano ya moja kwa moja (face-to- face interview) na wananchi katika ngazi ya kaya katika Mikoa yote Tanzania Bara na Zaznibar ambapo kaya takribani 7,800 zinatajiwa kufanyiwa mahojiano;
iv. Vikao vya majadiliano na makundi mbalimbali ya wadau ikiwemo Taasisi za Serikali, sekta binafsi, AZAKI, makundi maalum (wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu), vyama vya siasa nk na
v. Mahojiano mahsusi na viongozi pamoja na watu mashuhuri (Key Informant Interview).

10. Serikali ya Awamu ya Sita imeweka msukumo mkubwa wa maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 itakayozingatia:

i. Ukuaji wa uchumi utakaofungamanishwa na sekta za uzalishaji ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha chakula katika Bara la Afrika na duniani pamoja na kuongeza ajira;
ii. Kuimarisha sekta binafsi kwa kuwashirikisha katika mipango ya maendeleo na kutambua michango yao;
iii. Kuimarisha uwekezaji na usimamizi katika Mashirika ya umma ili kukizi ushindani ndani na nje ya nchi;
iv. Kuwa na jamii yenye maadili na yenye mazingira wezeshi ili kuweza kuvutia wawekezaji;
v. Kufungamanisha mipango ya sekta ili kuleta maboresho kupitia utekelezaji ulioratibika; na
vi. Ubainishaji wa viashiria hatarishi na mikakati yake ya utekelezaji.

**HITIMISHO**

11. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamelenga katika kuhakikisha malengo yote yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 yanakamilishwa na kufikiwa kupitia utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa.